



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI
(RITA)**



**UTARATIBU WA KUHAKIKI VYETI VYA KUZALIWA
NA VIFO KWA WAOMBAJI WA MIKOPO YA
ELIMU YA JUU 2018/2019**

Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhhamini (RITA) unapenda kuwafahamisha waombaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2018/2019 kuwa zoezi la Uhakiki wa Vyeti vya Kuzaliwa kwa waombaji, na vyeti vya vifo vya wazazi wa waombaji nchi nzima kama ambavyo tumekubaliana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) linaendelea kwa njia zifuatazo:

1. Mwombaji kuwasilisha nakala ya cheti katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya alikokipata Cheti cha Kuzaliwa;
2. Waombaji wanaoishi nje ya Wilaya walikopata Cheti cha Kuzaliwa pamoja na waliopo Mkoa wa Dar es Salaam, waingie katika mtandao kwa anuani: <http://uhakiki.rita.go.tz/uhakiki> ili kupata maelezo ya jinsi ya kutuma nakala ya cheti na risiti ya malipo. Baada ya uhakiki cheti kilichohakikiwa kitatumwa kupitia anuani ya mwombaji katika mtandao.

Ada ya Uhakiki kwa kila cheti ni TShs. 3,000/= (elfu tatu) ilipwe kupitia Benki ya NMB kwenye akaunti ya Administrator General Collection Account Na. 20610009881 au Benki ya CRDB kwenye akaunti ya Administrator General Collection Account Na. 0150339892600

Kila mwombaji awasilishe/atume kivuli cha cheti inayosomeka vizuri kwa ajili ya uhakiki ikiambatanishwa na nakala ya risiti ya malipo. Vile vile, utaratibu uliotajwa hapo juu utatumika kwa ajili ya kuhakiki vyeti vya vifo vya wazazi.

Aidha, Tunapenda kuwasisitiza waombaji wote kufuata utaratibu ulioelekezwa hapo juu ili kuepuka usumbufu.

Kwa maelezo zaidi piga simu namba 0800117482

Imetolewa na:

**Emmy Kalomba Hudson
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu - RITA**